East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Baadhi Ya Sifa Za Sauti Zoloto Zinazotumiwa Na Baadhi Ya Wahubiri Wa Kipentekosti Kuwasilisha Injili Na Umuhimu Wake

*Teresiah Nyambura[1*] na Prof. Peter Githinji, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100 Nairobi, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: feryltery@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*10 Aprili 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Kanisa za Kipentekosti, Kanisa zisizo za Kipentekosti, Sauti Zoloto, Uzolotaji, Wapentekosti, Wasikilizaji.*

**IKISIRI**

Makala haya yalilenga kubainisha baadhi ya vigezo vinavyobainisha sauti zoloto zinazotumiwa na baadhi ya wahubiri wa Kipentekosti kama mtindo wa kuwasilisha injili. Tulilenga waumini wa madhehebu tofauti ya Kipentekosti katika eneo la Gilgil katika kaunti ya Nakuru. Tulitumia mihimili miwili ya nadharia ya “Modeli ya Mtazamo wa Wasikilizaji” (Bell, 1984, 2014). Mhimili wa kwanza unadai kuwa Mtazamo wa wasikilizaji hutumika katika viwango vyote vya lugha iwe ni lugha moja au wingi lugha kwani haiangazii tu kubadilisha mtindo wa utamkaji wa sauti, bali pia uchaguzi wa jinsi ya kutamka sauti na upole wa mazungumzo. Mhimili wa pili hudai kuwa mtindo wa matumizi ya lugha katika uzungumzaji huwa chanzo cha mabadiliko katika mahusiano ya mazungumzo. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika kwa sababu ya urahisi wa kupata walengwa wa makala haya. Kiasa kikubwa cha data kilitokana na kanda za sauti za mahubiri mbalimbali kutoka kwa wahubiri tofauti. Hatimaye, kanda tatu ambazo wahubiri walizolota na tatu ambazo wahubiri hawakuzolota zilitumika. Kanda za mahubiri zilichujwa kwa kutumia programu ya PRAAT ili kupata sifa za kiakustika zinazobainisha sauti zoloto. Mbinu za hojaji, mahojiano na wahubiri binafsi, uchunzaji na mahojiano na makundi legwa zilitumika katika uchanganuzi na ufasili wa data. Matokeo ya utafiti yalibainisha vigezo vikuu vitano ambavyo ni kipimo cha hezi, urefu wa mawimbi ya sauti, kiwango cha desibeli, mpumuo wa sauti, kiwango cha tambo na tofauti kati ya fomanti ya kwanza na ya pili kama baadhi ya sifa zinazobainisha sauti zoloto za wahubiri wa Kipentekosti.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

**APA CITATION**

Nyambura, T. & Githinji, P. (2023). Baadhi Ya Sifa Za Sauti Zoloto Zinazotumiwa Na Baadhi Ya Wahubiri Wa Kipentekosti Kuwasilisha Injili Na Umuhimu Wake *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 68-83. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166.

**CHICAGO CITATION**

Nyambura, Teresiah and Peter Githinji. 2023. "Baadhi Ya Sifa Za Sauti Zoloto Zinazotumiwa Na Baadhi Ya Wahubiri Wa Kipentekosti Kuwasilisha Injili Na Umuhimu Wake". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 68-83. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166.

**HARVARD CITATION**

Nyambura, T. & Githinji, P. (2023) "Baadhi Ya Sifa Za Sauti Zoloto Zinazotumiwa Na Baadhi Ya Wahubiri Wa Kipentekosti Kuwasilisha Injili Na Umuhimu Wake", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 68-83. doi: 10.37284/jammk.6.1.1166.

**IEEE CITATION**

T. Nyambura & P. Githinji, "Baadhi Ya Sifa Za Sauti Zoloto Zinazotumiwa Na Baadhi Ya Wahubiri Wa Kipentekosti Kuwasilisha Injili Na Umuhimu Wake", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 68-83, Apr. 2023.

**MLA CITATION**

Nyambura, Teresiah & Peter Githinji. "Baadhi Ya Sifa Za Sauti Zoloto Zinazotumiwa Na Baadhi Ya Wahubiri Wa Kipentekosti Kuwasilisha Injili Na Umuhimu Wake". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Apr. 2023, pp. 68-83, doi:10.37284/jammk.6.1.1166.

## UTANGULIZI

Nia kuu ya mitindo ya ushawishi huwa kuibua hisia fulani kwa hadhira kwa madhumuni ya kuifanya hadhira kuchukua mtazamo fulani au kushikilia imani inayosababisha mielekeo au vitendo fulani. Viongozi wa kisiasa, kijamii na kidini, mawakili na wanahabari ni baadhi ya kategoria ambazo hutumia mitindo na mbinu za ushawishi kwa kiwango kikubwa. Lengo lao kuu huwa kuhakikisha ufanisi wa mawasiliano na matokeo bora katika utekelezaji wa malengo ya ujumbe. Katika mtazamo wa KiAristotle, mitindo ya ushawishi ilishughulikiwa katika vipengele vya ulumbi vya logos, ethos na pathos (Lin, 2019). Ushawishi wa kilogos hulenga urazini ambapo maamuzi hufikiwa kutokana na kuhakiki, kuchanganua, na kutumia mantiki (Mshvenieradze, 2013). Kipengele cha ethos, hushawishi kwa kutathmini ukweli, haki, uaminikaji, na maadili. Mwisho, ushawishi wa kipathos, hulenga kuchochoea hisia kwa kufanya mpokea ujumbe kujitambulisha na habari anazopokea ambazo huziona kuwa zina uwiano na maslahi yake. Makala haya yatashughulikia ushawishi katika muktadha wa dini tukiegemea kipengele cha pathos.

Dini hugawika hasa kwa misingi ya kiimani kama vile dini ya Kiislamu, Budha, Sikhi na dini ya Kikristo miongoni mwa zingine. Dini ya Kikristo ni dini ambayo msingi wa imani yao ni Yesu Kristo. Dini hii imegawika katika madhehebu tofauti tofauti ambayo hugawika katika makundi mawili makuu ambayo ni dini ya Kikatoliki na Waprotestanti. Waprotestanti wamegawika katika makundi mengi kama vile: Waadventista, Waanglikana, Wamethodisti, Wakalvinisti na Wapentekosti. Wapentekosti ni tawi moja katika kundi la makanisa ya kiinjilisti (Evagelical). Katika kundi la Kiinjilisti nchini Kenya, kuna madhehebu ya Kipentekosti na yale yasiyo ya Kipentekosti. Yale ya Kipentekosti ni kama vile, Full Gospel (FG), Kingdom Seekers (KS), Kenya Assemblies of God (KAG), Christian Fellowship Foundation (CFF) na Pentecostal Evagelical Fellowship of Afrika (PEFA). Nayo madhehebu yasiyo ya Kipentekosti ni kama vile, Seventh Day Adventist (SDA) na Orthodox.

Katika dini zilizo na utaratibu mahususi wa kuwasilisha ibada zao, lugha yao huwa na sheria za kuzingatiwa. Hii ni tofauti na wahubiri wa Kipentekosti ambao kwa mujibu wa Gichuki (2015) huwasilisha injili kupitia njia ya kiroho na hekima. Vilevile, mara nyingi wahubiri wa Kipentekosti wa Kiafrika hushawishiwa na wahubiri wainjilisti wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

kimataifa wanaohubiri kupitia televisheni ambao wana kipaji na mitindo ya kuvutia ya uwasilishaji. Kutopata mafunzo ya uhubiri na kanuni za lugha huwafanya wahubiri kuibua mikakati mbalimbali ya kutekeleza kazi yao ya kuhubiri kama vile kuchezacheza na kipengele cha pathos katika uwasilishaji wa injili. Uzolotaji wa wahubiri katika makanisa ya Kipentekosti nchini Kenya unaweza kueleweka katika muktadha huu. Hapa hatumaanishi uzolotaji ambao husababishwa na shida za koo, lakini kama mtindo wa kuzungumza unaotumiwa na wazungumzaji kimaksudi.

Kulingana na Hornibrook na wenzake (2018), matumizi ya sauti zoloto yalianza miaka ya 1960 hasa katika nchi ya Marekani kisha baadaye mtindo huu ulienea hadi ukawa mtindo unaotumika katika mazungumzo. Kwa ujumla, uzolotaji unatumika kwa wingi katika jamii ya sasa kutimiza malengo mbalimbali ya kimawasiliano. Katika kuchanganua jinsi uzolotaji umetumiwa kama mbinu ya ushawishi miongoni mwa wahubiri wa Kipentekosti nchini Kenya, makala haya yalidhamiria kuchambua sifa za kiakustika zinazobainika wakati wahubiri wa Kipentekosti wanazolota wanapotoa mahubiri yao.

## Diskosi ya Dini

Diskosi ya dini hujumuisha vipera, rejesta na aina mbalimbali za matini ambazo huwa na lengo la mawasiliano ya kidini (Adam, 2017). Lugha ya dini huwa tofauti sana na lugha inayotumika katika mazungumzo ya kawaida, jambo linalofanya iwe vigumu kufahamika na watu wasiouelewa usuli wa wahusika katika dini husika au muktadha wa kimatumizi wa lugha hiyo (King'ei, 1992). Kwa jumla, kuna mitindo bayana ya lugha ya dini ambayo huandamana na vipengele vingine vinavyoimarisha ulumbi kama vile utamkaji na uimbaji wa nyimbo, nahau, ishara, jazanda na kadhalika (Naeem na wenzake, 2014). Dini mbalimbali huwa na mitindo yao ambayo nia yao huwa kuwashawishi waumini na kuwafanya washikilie imani zao na wazidi kujiimarisha kiimani. Wamarekani Weusi wana mbinu za kipekee ambazo zimeibua mitindo ya uwasilishaji injili yenye upekee (Similly, 2012). Akiunga mkono, Smitherman (1996) alieleza kuwa mtindo wa mahubiri miongoni mwa Wamarekani Weusi una sifa zake bayana ambazo zinatofautiana na za wahubiri wengine. Smitherman aliendelea kudau kuwa mitindo iliyotumika katika kanisa za Wamarekani Weusi ingepata nafasi kutumika katika matumizi ya kawaida. Kwa upande mwingine, mitindo ya uzungumzaji wa kawaida ilikuwa ikipenya katika mazingira ya kanisa. Uhusiano huu wa uwili ndio dhihirisho la umuhimu wa kuliangazia suala la mitindo ya dini kama mojawapo ya vipengele vinavyoleta ukamilisho wa mitindo ya mawasiliano ya jamii.

Mitindo ya litajia imeangaziwa na Crystal (1969), Holt (1972), Ndung'u (2001), Waweru (2014), Omowumi na Soku (2015). Wasomi hawa wanadai kuwa lugha ya litajia yafaa iwe lugha isiyo ngumu, fiche na isiyo na urasmi kwani haizingatii sheria za kisarufi. Waliendelea kudai kuwa sajili hii ni ya kipekee na yafaa ikidhi mahitaji ya mhubiri na waumini ili lengo la wasilisho hilo litimie. Hili lilionekana wazi katika utafiti wa Waweru (2014) aliyedai kuwa kubadilisha msimbo husaidia mhubiri kuhakikisha uhusiano wake na waumini umeimarika na lengo lake linatimia. Ndung'u (2001) alichanganua usemi katika sajili ya dini na sifa bainifu za lugha ya mahubiri na kubaini kuwa wahubiri wengi walichagua lugha watakayoitumia hasa katika mwanzo wa injili ili kuleta uhusiano mwema kati yao na waumini wao. Kama anavyodai Loveday (1983), mianzo ya mazungumzo si mbinu zisizo na maana na mianzo hiyo huwa na athari katika mazungumzo yanayofuata. Anaendelea kudai kuwa kuna ruwaza katika mianzo ya mazungumzo ambazo ni matumizi ya maswali, mifano katika kuelezea ujumbe, takriri, ishara na matumizi ya sauti.

Matumizi ya mtindo tofauti wa mahubiri katika dini tofauti kama vile ya Kikatoliki na Kipentekosti iliungwa mkono na Brown (1963) alipodai kuwa,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

lugha ya uwasilishaji wa injili inaweza kubainisha wahubiri tofauti. Kwa upande mwingine, lugha iliyotumika katika kanisa za Kipentekosti ilitafitiwa na Omowumi na Soku (2015) ambao waliangazia ufundi wa lugha katika uwasilishaji wa mahubiri. Walibaini kuwa makasisi walitumia vipengele vingi vya sauti katika kuzungumza, tofauti na makasisi wa Kikatoliki. Kutokana na data waliyoipata, waliripoti kuwa waumini wengi walipendelea wahubiri ambao hutumia vipengele hivyo. Hata hivyo, si wote walikubaliana na suala hili kwani baadhi yao walidai kuwa hawaelewi vyema na kuwa makasisi ambao wanatumia mitindo hii huonekana kuwa wenye majigambo. Kwa vile utafiti huu haukutaja ni kigezo kipi hasa katika kipengele cha sauti walichokitafiti, makala haya yanalenga zaidi mitindo hiyo ya vipengele vya sauti na hasa kipengele cha uzolotaji kama mtindo unaotumiwa na wahubiri wa Kipentekosti kuwashawishi waumini wao.

**Matumizi ya Mtindo wa Uzolotaji Katika Mawasiliano**

Kulingana na Hornibrook na wenzake (2018), matumizi ya sauti zoloto yalianza miaka ya 1960 hasa katika nchi ya Marekani kisha baadaye mtindo huu ulienea hadi ukawa mtindo unaotumika katika mazungumzo. Hapo awali, mtindo huu ulitumika na wanaume wa Kimarekani lakini katika karne ya 20, wanawake walianza kuutumia kama njia ya kuakisi mamlaka katika mazingira ya kazi (Sorokowski & Wengine, 2019). Baadaye, uzolotaji ulikuja kutumiwa pia na jinsia ya kike katika mawasiliano yao kama njia ya kujitambulisha na kikundi fulani (Yuasa, 2010; McAlpine, 2016).

McAlpine (2016) alidai kuwa uzolotaji ulitumiwa kwa wingi na wanawake wa Kimerekani, wanaosoma katika chuo kikuu. Madai haya yanakubaliana na utafiti wa Hornibrook na wenzake (2018) ambao walitafiti matumizi ya sauti zoloto miongoni mwa wanawake wa Marekani. Wakichunguza uzungumzaji wa mwigizaji Scarlet Johansson, Shaw na Crocker (2015) walibaini kuwa alipoigiza uhusika wa Kimarekani alitumia uzolotaji mwingi kuliko ule wa uhusika wa Uingereza na kuwa uzolotaji ulijitokeza wazi akiigiza matukio ya kimapenzi. Johansson alitumia uzolotaji kama njia ya kukidhi nafasi yake katika ulimwengu wa uigizaji na kujiweka katika kikundi fulani ambacho kinaathiriwa na uhusika wake. Pia, walibaini kuwa mtindo huu ulitumika pakubwa na ulitumika kama njia ya kipekee ya kuwashawishi wasikilizaji wa mazungumzo yoyote yale.

Wakirejelea tafiti za wasomi mbalimbali, Hornibrook na wenzake (2018) wanadai wasomi huwa na maoni tofauti kuhusu uzolotaji unaotumiwa na wanawake katika mitandao ya kijamii. Unaweza kutumika kuonyesha ukosefu wa ujasiri, kuwa na ujasiri mwingi au pia kuonyesha dhana ya kuakisi mamlaka. Baadhi ya wazungumzaji wa Kiingereza walishikilia kuwa uzolotaji katika mazungumzo huakisi mamlaka ilihali wengine walipinga mtindo huu wakisema ni mtindo chapwa usio na msingi wowote ule wa kutumika katika mazungumzo. Kuakisi hili, Hornibrook na wenzake waliangazia utafiti wa Anderson na wenzake (2014) ambao walitafiti uzolotaji katika kiwango cha kitaifa wakiangazia mamlaka ya ulimwengu wa kibiashara. Walibaini kuwa uzolotaji una athari hasi na pia huonyesha kuwa mzungumzaji si msomi na uzungumzaji wake haupendeki.

Watafiti wengine kama vile Wolk na wenzake (2012) wanaamini kuwa matumizi mengi ya uzolotaji yamechangiwa na mwimbaji Britney Spears na mwanamitindo Kim Kardashian. Haya yakubaliana na utafiti wa Hildebrand-Edgar (2014) aliyetafiti kuhusu sauti zoloto kama amali ya kuakisi mamlaka. Hildebrand-Edgar alidai kuwa wazungumzaji walitumia uzolotaji zaidi wakiwasiliana na wale wasio na uhusiano wa karibu nao. Pia, uzolotaji ulitumika kuwasilisha jambo ambalo walikuwa na uhakika au wasio na uhakika nalo, jambo ambalo wameshaliona au wameshalipitia ili kuakisi mamlaka katika usemi huo. Kulingana naye, kigezo kikuu cha uzolotaji ni

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

uhusiano ulionao na wale unaowasiliana nao au hali ambayo imezunguka mawasiliano hayo kama vile kuwa na uhakika wa kile unachokisema. Aidha, kuna uzolotaji wa kawaida ambao hutokea kulingana na sauti ambazo zinatamkwa hivyo na kuna uzolotaji usio wa kawaida, yaani kama mtindo wa kuzungumza ambao hutegemea uhusiano wa kijamii.

Vilevile, matumizi ya sauti zoloto na Lady Gaga katika mazungumzo yake yamechunguzwa na Esposito (2015). Esposito alipata kuwa Lady Gaga alikuwa mwangalifu katika mazungumzo yake ndiposa akawa anatumia sauti zoloto kwa wingi katika mazungumzo mengine na mengine kuwa na uzolotaji wa kiwango cha chini. Aidha, alifanya hivyo kwa ajili ya kujenga mtazamo wa hisia za kimapemzi na pia kuleta dhana ya hulka ya uwazi na ukweli kwa wasikilizaji wake. Pia alibaini kuwa mzungumzaji anaweza kutumia mitindo tofauti katika mazingira tofauti ya mazungumzo huku akitumia uzolotaji mwingi anapozungumzia mada ambayo imejawa na hisia za kupenda kinachojadiliwa au mada zinazomhusu yeye binafsi. Hivyo basi, ijapokuwa uzolotaji ni njia moja ya utoaji sauti (Ladefoged & Johnson, 2011), umetumika na watu mbalimbali katika miktadha tofauti kama mtindo unaolenga kutekeleza majukumu fulani ya kimawasiliano. Lengo letu katika makala haya ni kuangazia matumizi yake katika diskosi ya dini kama unavyotumika na wahubiri wa Kipentekosti.

## Utoaji wa Sauti Zoloto

Kulingana na Ladefoged na Johnson (2011), uzolotaji hutokea wakati nyuzi za sauti huja pamoja hivi kwamba zinarindima katika upande wa mbele. Mrindimo unaotokea huwa wa polepole na huleta mkazo wa sauti ambao husababisha uzolotaji. Wakijikita katika lugha ya Kichina, Belotel-Grenié na Grenié (1994, 2004) wanaelezea kuwa katika utoaji wa sauti zoloto, nyuzi za glota huwa zimekazana upande wa nyuma huku zikirindima polepole katika upande wa mbele. Wanaendelea kusema kuwa uzolotaji hudhihirisha nguvu nyingi katika kasi mawinbi za juu kwa sababu nyuzi sauti hujikaza na kujifunga haraka kwa kila mzunguko wa glota. Sauti zoloto humaanisha utoaji wa sauti mseto ambazo hutolewa kwa namna tofauti, hivyo kuwa na sifa mbalimbali wanavyodai Keating na wenzake (2015). Kulingana nao, sifa za uzolotaji bora huwa mrindimo wa chini wa nyuzi za sauti, mirindimo mirefu na mifupi na vilevile glota hufunguka kiasi tu na kufungika kwa muda mrefu huku hewa kidogo tu ikiruhusiwa kupita. Hata hivyo, kuna sifa zingine kama vile mpumuo mnyonge na mfupi wakati wa kutamka sauti ambao hubainisha jinsi sauti zoloto itatolewa. Hii ndiyo sababu ya kuwa na aina tofauti za sauti hii kwani sauti hizi huchukua sifa zake mahususi.

Ladefoged na Johnson (2011) na Keating na wenzake (2015) wanaungwa mkono na Bellavance (2021) katika utafiti wa uzolotaji katika uzungumzaji wa vijana kutoka Vermont. Watafiti hawa walibaini kwamba sauti zoloto hutolewa haswa wakati hewa inasimama katika glota na wanadai kwamba uwekaji wa mpumuo katika sauti zoloto ni ubunifu unaoendelezwa na kusimama kwa hewa katika glota. Pia wanadai kuwa uzolotaji ni mseto wa hewa inayosimama katika glota na huhusishwa katika kufunguka kwa glota ili iwachilie sauti zoloto.

Wanaisimu wa hapo awali kama Ferdinand de Saussure, Noam Chomsky na Baudouin de Courtenay ambao wametajwa na Keating na wenzake (2015) walidai kuwa katika utoaji wa sauti zoloto, kuna mshinikizo wa hewa ulio chini na hewa kutembea polepole katika nyuzi za sauti zilizokazwa na mrindimo wa nyuzi hizi huwa mfupi, wa chini au hata ambao si wa kawaida. Baadaye, sifa zaidi ziligunduliwa kama vile kuwa na kipimo cha urefu wa mzunguko wa mawimbi ya sauti kisicho cha kawaida na kufungwa kwa nyuzi za sauti bila ya kutarajiwa. Hedelin na Huber (1990) wanaongeza kuwa sauti zoloto hutolewa wakati kuna mpumuo usio wa kawaida. Kwa vile kila lugha huwa na mpangilio wa kipekee wa sauti zake,

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

tulidhamiria kuchunguza kuhusu sifa ambazo zinajibainisha katika uzolotaji wa wahubiri wa kipentekosti kasa wanapohubiri kwa Kiswahili.

## MISINGI YA NADHARIA

Nadharia ya mtazamo wa msikilizaji inayoangazia namna wazungumzaji hujinasibisha na mitindo ya uzungumzaji wa wasikilizaji inahusishwa na Allan Bell (1984, 2014). Inadai kuwa wazungumzaji hubadili uzungumzaji wao kwa kutilia maanani wahusika wao ili kuleta uwiano na wasikilizaji na pia huongoza uteuzi wa namna au lugha ya kutumia katika maongezi yao. Katika utafiti wake wa vituo vya redio, Bell alibaini kuwa watangazaji wale hale walizungumza kwa namna tofauti kwa kuzingatia wasikilizaji wao wa redio husika. Kulingana na Bell, hili lilitokana na kuwa watangazaji walibaini matarajio ya wasikilizaji kwa kuwa mada ilikuwa ni ile ile moja. Nadharia hii ina mihimili kuu tisa lakini katika makala haya tutazingatia mhimili wa nne na wa nane pekee. Mhimili wa nne unadai kuwa mtazamo wa wasikilizaji hutumika katika viwango vyote vya lugha iwe ni lugha moja au wingi lugha kwani haiangazii tu kubadilisha mtindo wa utamkaji wa sauti, bali pia uchaguzi wa jinsi ya kutamka sauti na upole wa mazungumzo. Pia unaangazia ubadilishanaji wa mtindo kutoka lugha moja hadi nyingine. Hii yamaanisha kuwa mzungumzaji anaweza kubainisha vigezo vyote vya lugha atakavyovitumia katika uzungumzaji wake mradi tu lengo lake litimie.

Mhimili wa nane wa nadharia ya Bell (1984, 1997) unadai kuwa mtindo wa matumizi ya lugha katika uzungumzaji huwa chanzo cha mabadiliko katika mahusiano ya mazungumzo. Katika mhimili huu, vigezo tofauti vya lugha hutumiwa ili kubadili mitindo ya uwasilishaji wa ujumbe. Kwa vile lugha hujisimamia na huongoza mawasiliano, wazungumzaji wanaweza kubadilisha mitindo ya lugha ili kukidhi mahitaji yao. Mhimili huu ulisaidia kubainisha vigezo vya mtindo wa uzolotaji ambavyo hutumiwa na wahubiri wa Kipentekosti wanapowasilisha injili.

Kwa kuzingatia mihimili hii, tunadai kuwa uzolotaji kama kipengele cha ulumbi cha pathos kinachotumika na wahubiri wa Kipentekosti kinajidhihirisha katika kiwango cha kifonetiki na sifa zake zinaweza kufafanuliwa kiakustika. Wahubiri wanapotumia uzolotaji kama mtindo wa ushawishi wa waumini wao, wanafanya hivyo kukidhi matamanio ya wasikilizaji wao ambao wananasibisha uzolotaji na mamlaka ya mtoa ujumbe.

## MBINU ZA UTAFITI

Kanda nyingi za mahubiri yaliyonaswa kutoka kwa vyombo vya habari zilisikilizwa na kuchunjwa. Kanda zingine za mahubiri zilinaswa kutokana na uchunzaji katika ibada za madhehebu ya Kipentekosti. Kanda zenye uzolotaji zilitenganishwa na zisizo na uzolotaji. Kutokana na hili, kanda sita zilichaguliwa ambapo tatu zilikuwa na mahubiri ambayo yaliwasilishwa kutumia mtindo wa uzolotaji na tatu ambazo mtindo huo haukutumika katika uwasilishaji wa mahubiri. Hizi ndizo kanda ambazo zilitumika katika utafiti huu na kila kanda ilikuwa kati ya sekunde 30-40. Program ya PRAAT ambayo hutumiwa kuchunguza sauti zilizorekodiwa ilitumika kukokotoa data ambazo zilitumika katika utafiti huu. Tutafafanua kwa kifupi yaliyomo katika kila kanda iliyotumika. Kanda zote zilinaswa kutoka kwa wahubiri wa kiume ili kuzuia jinsia kuwa kigeu kiingilizi.

Pia, mbinu ya mahojiano ilitumika kwa wahubiri wa kanisa za Kipentekosti ambao watatu kati yao huzolota na watatu hawazoloti wanapohubiri. Zaidi ya hayo, makundi lengwa matatu ya waumini wa kanisa za Kipentekosti yalitumika na kila kikundi kilikuwa na wahojiwa wanne. Uteuzi huu ulitegemea vigezo tofauti tofauti ambavyo vilitumika katika kuteua watafitiwa hawa. Wakati wa mahojiano mtafiti alinakili hoja za watafitiwa huku akinasa sauti zao. Mahojiano haya yalikuwa ya faragha ili kila mtafitiwa awe na fursa mwafaka ya kujieleza kikamilifu. Juu ya hayo, mbinu ya hojaji ilitumika ambapo wasailiwa mia moja ishirini

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

walihitajika kujibu maswali kuhusu sauti ambazo wahubiri wao hutumia wanapohubiri. Zaidi ya hayo, mbinu ya hojaji ilitumika kwa watafitiwa mia moja ishirini ambao walipewa maswali wazi na maswali funge. Kwa maswali wazi, mtafitiwa alihitajika kutoa maelezo yake binafsi ilhali kwa funge, mtafitiwa ilibidi ajibu kulingana na swali husika.

### Kanda Ambazo Mtindo wa Uzolotaji Umetumika

*Kanda 1*

Mahubiri haya yalirejelea Biblia kutoka kitabu cha Isaiya 6:5. Mahubiri haya yalifanyika katika mandhari ya kanisa. Mada ilikuwa juu ya haja ya maneno ambayo waumini wanayatoa midomoni mwao yawe maneno mema ya Kiungu ili uhusiano wao na Mungu uimarike. Mhubiri anarejelea nabii Isaiah ambaye anasema kwamba midomo yake ni michafu na anaishi katikati ya watu wenye midomo michafu.

*Kanda 2*

Mhubiri anarejelea Biblia kutoka kitabu cha Wakorintho wa 1 sura ya 12: 4-11. Mahubiri haya yalifanyika kwenye televisheni ya NYTV na yalipeperushwa moja kwa moja kutoka mandhari ya kanisa. Mada ilikuwa juu ya vipaji vya Roho Mtakatifu ambavyo huzaa matunda kama vile uvumilivu, upole, furaha na mapendo ambayo humfanya mwanadamu kuishi vyema.

*Kanda 3*

Mahubiri yalitolewa katika Ufunuo 1:7. Kanda hii ilipakuliwa kutoka mtandaoni na mhubiri alikuwa akitembeatembea jukwaani alipohubiri. Mada yake ilihusu ujio wa Mwanakondoo wa Mungu ambapo akija duniani kila jicho litamwona na kutakuwa na utawala mmoja ulio na usawa.

### Kanda Ambazo Mtindo wa Uzolotaji Haukutumika

*Kanda 1*

Mahubiri haya yalirejelea Biblia kutoka kitabu cha I Wakorintho 15:1-2. Mada ilikuwa jinsi ya kujitetea mbele ya Mungu. Mhubiri alipohubiri sauti yake ilikuwa sauti yenye upole na unyenyekevu.

*Kanda 2*

Mahubiri haya yarejelea Bibilia kutoka kitabu cha Amos 5:4-6. Mahubiri haya yalipakuliwa kutoka mtandaoni. Mada ilihusu siri ya kuutafuta uso wa Mungu ili mwanadamu aweze kutimiza lengo lake mahususi aliloitiwa. Baada ya kufanya hivyo, ataweza kupambana na vikwazo vyovyote ambavyo atapatana navyo. Mhubiri alihubiri akiwa amesimama mahali pamoja.

*Kanda 3*

Mahubiri haya yametolewa katika Kitabu Kitakatifu cha Biblia kutoka Yeremia 15:19 na Yakobo 3:11. Yalipakuliwa mtandaoni na mada ilihusu ulimi ambao ni chemichemi ambayo inafaa kutumiwa vyema ili maombi ya Mkristu yasikike katika ulimwengu wa Kiroho. Ili haya yatendeke, ni lazima Mkristo atakase ulimi wake. Mhubiri alihubiri huku akitembeatembea jukwaani.

### Vigezo Vinavyobainisha Sauti Zoloto ya Wahubiri wa Kipentekosti

Baada ya kuzibadilisha kanda hizi kidijitali kwa kutumia programu ya PRAAT, kulikuwa na tofauti bayana kati ya kanda ambazo wahubiri walizolota na zile ambazo wahubiri hawakuzolota. Baadhi ya vigezo vilivyotumika katika kubainisha sifa za uzolotaji wa wahubiri wa Kipentekosti ni: kipimo cha Hezi, urefu wa mawimbi, kipimo cha urefu wa mawimbi ya sauti, mpumuo, kiwango cha tambo, tofauti kati ta fomanti ya kwanza (F1) na fomanti ya pili (F2) na sifa nyinginezo za sauti hizo kutokana na maelezo ya wasailiwa.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

**Kipimo cha Hezi (Hz)**

Hezi (Hz) ni kipimo kinachopima jinsi sauti hutamkwa aidha kwa sauti ya chini au sauti ya juu. Ni kipimo cha kasimawimbi ambacho huonyesha mzunguko mmoja kwa sekunde moja kutoka sehemu fulani ya utamkaji wa sauti. Mizunguko mingi kwa muda wa sekunde moja kutoka sehemu moja hadi nyingine, husababisha mtetemo wa kasi na huashiria kidatu cha juu na ikiwa michache kwa sekunde moja, husababisha mtetemo wa polepole kuashiria kidatu cha chini. Sauti ya hezi moja humaanisha kuwa wimbi moja hupitia sehemu fulani kwa muda wa sekunde moja. Kwa kawaida, binadamu anaweza kusikia sauti kutoka hezi 20 hadi kilohezi 20 (Møller & Pedersen, 2004).

Keating na wenzake (2015) wametambua mtetemo wa nyuzi za sauti kuwa mojawapo ya sifa za uzolotaji. Katika utafiti wetu, ilibainika wazi kwamba sauti zenye kipimo cha chini cha hezi zilikuwa na uwezekano mkubwa wa kuwa sauti zoloto kwani zinapotamkwa sauti huwa nzito ilihali zile ambazo zilitamkwa sauti ikiwa nyepesi na ya juu ni sauti ambazo hazina uzolotaji. Hii yakubaliana na mawazo ya Keating na wenzake (2015) ambao wanadai kuwa sauti zoloto husababishwa na mirindimo ya chini ya nyuzi za sauti ambazo huwa fupi, mrindimo ulio wa chini au hata mrindimo ambao si wa kawaida hutolewa. Mirindimo hii hufanya sauti inayotamkwa kuwa ya kiwango cha chini.

**Jedwali 1: Kielelezo cha Hezi**

| KANDA | Kanda zenye uzolotaji | Kanda ambazo hazina uzolotaji |
|---|---|---|
| 1. Juu | 240 Hz | 324.4 Hz |
| Chini | 76.6 Hz | 75.5 Hz |
| 2. Juu | 470.7 Hz | 497.7 Hz |
| Chini | 76.5 Hz | 86 Hz |
| 3. Juu | 479.1 HZ | 201.3 Hz |
| Chini | 103.8 Hz | 103.2 Hz |
| Jumla Juu | 1,189.8 HZ | 1,023.4 Hz |
| Chini | 259.1 | 264.7 Hz |
| Wastani Juu | 396.6 Hz | 341.1 Hz |
| Chini | 86.4 Hz | 88.23 Hz |

Matokeo ya kanda hizi yalifanyika kuanzia sekundi 0 hadi sekunde 5 za kanda hizi kwa sababu programu ya PRAAT haingekokotoa kanda ya sekunde arubaini. Kutokana na hili, matokeo haya yanajikita katika sehemu hiyo ya mahubiri kama ifuatavyo; Jumla ya kipimo cha juu cha hezi kwa kanda tatu zenye uzolotaji ni Hz 1,189.8 9 na chini ni 259.1. Hapa tunapata kipimo cha wastani juu kikiwa Hz 396.6 na wastani chini ukiwa Hz 86.4.

Katika kanda ambazo hazina uzolotaji, jumla ya kipimo cha juu ni Hz 1023.4 na chini ni Hz 264.7. Hii inatupa wastani juu wa Hz 341.1 na wastani chini wa Hz 88.23. Data hii inaonyesha, kuwa kuna tofauti bayana kati ya kanda zenye uzolotaji na zile zisizo na uzolotaji. Tunaona pia kuwa wastani chini wa kanda zisizokuwa na uzolotaji unazidi wa zile zenye uzolotaji kwa Hz 1.83. Kwa upande mwingine, watani juu wa kanda zenye uzolotaji ni mkubwa kuliko zile zisizo na uzolotaji kwa Hz 55.5 kumaanisha uzolotaji unabainishwa na kipimo cha juu cha hezi.

**Urefu wa Mawimbi ya Sauti**

Sifa nyingine inayobainisha sauti zoloto ni kipimo cha kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti katika utamkaji. Kanda ambazo zilikuwa na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

uzolotaji zilikuwa na mawimbi marefu ikilinganishwa na zile ambazo zilitamkwa bila uzolotaji. Hata hivyo, mawimbi ya sauti hayakudhihirisha utaratibu wowote kwa vile kulikiwa na yale yaliyokuwa mafupi na mengine yaliyokuwa ni marefu. Hili lilifanya sauti zisiwe na mirindimo isiyo ya kawaida. Hebu tuzingatie data katika kilelezo 1, (a) na (b)

**Kielelezo 1: Mawimbi ya Sauti**

**a) Kanda zenye uzolotaji**

**Kanda 1**



**Kanda 2**



**Kanda 3**



Haya ni mawimbi ya sekunde arubaini ya kanda zote tatu ambazo zimezolotwa. Kutokana na mawimbi haya, kanda 2 ilikuwa na mawimbi marefu ikilinganisha na mawimbi ya kanda 1 na 3 kwani mawimbi ya sauti hiyo yalikuwa marefu sana na mengi.

**b) Kanda bila uzolotaji**

**Kanda 1**



**Kanda 2**



**Kanda 3**



Kutokana na mawimbi haya, ni bayana kuwa mawimbi ya kanda bila uzolotaji ni mafupi yakilinganishwa na ya sauti ya kanda ambazo zimezolotwa. Mawimbi ya kanda 2 yanaonekana kuwa mengi na marefu kwa sababu nguvu sauti ambazo mhubiri huyu alitumia zilikuwa nyingi zaidi ikilinganishwa na kanda 1 na 3. Katika kanda 3, mhubiri alihubiri kwa upole na utaratibu fulani ambao uliathiri utoaji wa sauti. Hata hivyo, tunaona kuwa mawimbi ya sauti katika kanda zenye uzolotaji ni marefu zaidi ikilinganishwa na urefu wa mawimbi ya sauti ya kanda ambazo hazijazolotwa. Pia, ilibainika kuwa urefu wa mawimbi na utoaji wa sauti zoloto au isiyo zoloto kwa kiwango fulani ulitegemea mtindo na hulka ya mtu binafsi, nguvu sauti aliyoitumia katika utamkaji wa sauti husika na kutosoma mahali pamoja katika Biblia, kwa hivyo tofauti ya maudhui katika vifungu walivyosoma ziliweza kuchangia tofauti ya mawimbi ya sauti.

### Mpumuo

Ilibainika wazi kuwa uzolotaji mwingi ulitokea wakati ambapo mzungumzaji alizungumza kwa kufululiza na hivyo kuathiri wakati wa kupumua

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

ambao ulikuwa ni mfupi sana na usio wa kawaida. Hii ilijidhihirisha kupitia mawimbi ya sauti za wahubiri waliozolota kwani wahubiri hawa walizolota zaidi pale ambapo walizungumza kwa kufululiza, jambo ambalo ni tofauti na uzungumzaji wa kawaida. Hii inakubaliana na madai ya Keating na wenzake (2015) kuwa uzolotaji hutokea wakati ambapo glota hufunguka kiasi tu na kufungika kwa muda mrefu huku hewa kidogo tu ikiruhusiwa kupita, hivyo kuwa na mpumuo usio wa kawaida.

**Kielelezo 2: Mawimbi ya Sauti-Mpumuo wa Sauti**

**Picha 1: Kanda 2 yenye uzolotaji**



**Picha 2: Kanda 3, bila uzolotaji**



Katika *Kielelezo 2*, mpumuo unaonyeshwa na sehemu ambazo ni mstari usio na mawimbi, yaani, mapengo kati ya kundi la mizunguko ya mawambi sauti. Katika *Picha 1* (kanda 2) ni bayana kuwa mhubiri alifululiza maongezi yake bila ya kuwa na nafasi ya kupumua, uzolotaji mwingi ulitokea kutokana na kuathirika kwa muda wa kawaida wa kupumua alipotamka sauti zake. Hii ni tofauti na *Picha 2* ambapo mhubiri alihubiri kwa kawaida bila ya kuathiri muda wa kupumua alipotamka sauti zake.

Pia pana tofauti katika muda wa kupumua katika kanda hizi. Hii yajitokeza wazi ambapo muda wa kupumua (baada ya kutamka sauti na kabla ya kutamka sauti) ni mrefu katika kanda 2 (3) ambayo haijazolotwa ikilinganishwa na kanda ambayo imezolotwa kwani muda huo ni mfupi. Kutokana na hili, inabainika wazi kwamba kanda 2 (3) ambayo haijazolotwa ina mipumuo mingi na ya kawaida ikilinganishwa na kanda 2 (2) ambayo imezolotwa ambayo ina mipumuo mitatu tu kumaanisha kuwa palikuwa na mfululizo mwingi katika kuzungumza katika kanda hii, kinyume na kanda ambayo haijazolotwa ambapo mhubiri alipumua mara kwa mara katika mazugumzo yake.

### Kipimo cha Tambo (Amplitude)

Kwa mujibu wa González na wenzake (2016, uk. 5), tambo la wimbi sauti ni umbali wa kiwango cha juu ambapo chembe au kitu husonga kuelekea kila pande kutoka sehemu moja, yaani, kutoka msingi wake au sehemu ya chini kabisa hadi sehemu ya juu katika kilele cha pindo lake. Tambo likiwa la kipimo cha juu ndivyo sauti husikika ikiwa ya juu zaidi. Kielelezo 3 hapa chini kinaonyesha tofauti za matambo ya kanda ya mahubiri ya mhubiri aliyezolota na yule ambaye hakuzolota.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

**Kielelezo 3: Kipimo cha tambo**

**Kanda 1 (haijazolotwa)**



**Kanda 2 (imezolotwa)**



Sauti zinapotamkwa huwa na tambo la juu au la chini kutegemea jinsi sauti inavyotamkwa. Sauti zoloto huwa na matambo ya juu katika wimo wa juu na wa chini kutoka sehemu ya msingi (yaani sufuri). Kielelezo 3 kinaonyesha kanda 1 ina matambo ya juu na ya chini ambayo ni mafupi ikilinganishwa na kanda 2 ambayo matambo yake ya juu na ya chini ni marefu mno. Jedwali 2 hapo chini linaonyesha viwango vya matambo ya juu na ya chini vya kanda zote sita. Matokeo haya yanaanzia sekundi 0 hadi sekunde 5 za kanda hizi kwa sababu programu ya PRAAT haingeweza kuzichanganua zikiwa ni za sekunde arubaini.

**Jedwali 2: Kielelezo cha Matambo**

| Kanda | Kanda Zenye Uzozolotaji | Kanda Bila Uzolotaji |
|---|---|---|
| 1. Juu | 0.24 | 0.27 |
| Chini | -0.15 | -0.50 |
| 2. Juu | 0.97 | 0.75 |
| Chini | -0.10 | -0.70 |
| 3. Juu | 0.89 | 0.30 |
| Chini | -0.88 | 0.38 |
| Jumla Juu | 2.1 | 1.32 |
| Chini | -1.13 | -0.82 |
| Kiwango wastani Juu | 0.7 | 0.44 |
| Chini | -0.38 | -0.27 |

Kutokana na jedwali hili, kanda ambazo wahubiri walizolota zilikuwa na jumla ya matambo ya juu ya 2.1 na matambo ya chini ya -1.13, nazo kanda ambazo hazijazolotwa zilikuwa na jumla ya matambo ya juu ya 1.32 na ya chini ya -0.82. Wastani wa juu cha kanda zilizozolotwa ni 0.7 na wa chini ni -0.38. Kwa upande mwingine, kanda ambazo hazijazolotwa zina kipimo cha wastani wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

juu cha tambo cha 0.44 na cha wastani wa chini cha -0.27. Kutokana na haya, inabainika kwamba sauti zoloto huwa na matambo ya kiwango cha juu zaidi kwani mawimbi yake huwa marefu na nguvu sauti ya kutamka sauti hizo huwa juu. Hii husababisha matambo yawe ya juu zaidi ikilinganishwa na sauti ambayo haijazolotwa kwa sababu matambo yake huwa ya kiwango cha chini.

**Tofauti Kati ya Fomanti ya Kwanza (F1) na Fomanti ya Pili (F2)**

Fomanti huonyesha nguvu sauti zilizotumika kutamkia sauti husika. Formati mara nyingi hutumika kuchanganua irabu. Kuna fomanti nne ambazo ni F0, F1, F2, F3 na F4. F0 ni kiwango wastani cha jumla cha formanti. F1 hutegemea urefu wa ulimi hivi kwamba irabu ambayo huwa na formanti ya juu ni irabu ambayo hutamkwa ulimi ukiwa chini na ile ambayo huwa na fomanti ya chini hutamkwa ulimi ukiwa juu ya kinywa. F2 hutegemea utamkaji wa irabu katika sehemu ya nyuma ya irabu. Nayo F3 hutegemea jinsi midomo imeviringwa wakati wa kutamka sauti mahususi. Kulingana na Ladefoged na mwenzake (2001), fomanti za 3 na 4 kwa kawaida hazitumiki sana kwa sababu vipimo vyake ni vya juu zaidi. Fomanti husaidia kutamka namna tofauti za irabu hivyo kuwa na mitindo tofauti kwani mzungumzaji anaweza kubadilishabadilisha fomanti hizi apendavyo ili kuleta tofauti za kimtindo katika mazungumza yake.

**Jedwali 3: Kielelezo cha F1 na F2**

| Kanda | | Kanda Zenye Uzolotaji | Kanda Bila Uzolotaji |
|---|---|---|---|
| Kanda 1 | F1 | 441 | 433 |
| | F2 | 1659 | 1430 |
| Kanda 2 | F1 | 538 | 584 |
| | F2 | 1324 | 1581 |
| Kanda 3 | F1 | 409 | 705 |
| | F2 | 1374 | 2942 |
| Jumla | F1 | 1388 | 1722 |
| | F2 | 4359 | 5953 |
| Wastani | F1 | 462.6 | 574 |
| | F2 | 1453 | 1984 |

Kutokana na haya, F1 ya kanda zote tatu ambazo zimezolotwa ilikuwa ni 1388 na kipimo wastani ni 462.6, nayo F2 katika jumla ya kanda zote tatu ni 4359, kipimo cha wastani ni 1453. Vilevile jumla ya vipimo vya F1 na F2 vya kanda ambazo hazijazolotwa ni 1722 na 5953 mtawalia kwa wastani ni 574 na 1984 mtawalia. Hii inaonyesha kwamba sauti zoloto inapotamkwa, sifa yake moja ni kuwa ni sauti ya chini. Hii inajidhihirisha kupitia kipimo wastani cha F1 cha sauti zoloto ambacho ni 462.6 ikilinganishwa na F1 ya sauti ambazo hazijazolotwa ambacho ni 574. Tofauti za kipimo wastani cha sauti hizi ni 111.4. Pia kipimo wastani cha F2 cha sauti zoloto ni 1453 nayo F2 ya sauti ambazo hazijazolotwa ni 1984. Hii yadhihirisha kwamba sauti zoloto hutamkwa kwa sauti ya chini hivyo kuibua sifa nyingine ya sauti zoloto. Matokeo haya yakubaliana na utafiti wa Samely (1991) anayedai kuwa sauti zoloto huwa na F1 na F2 ambazo ni za chini katika lugha ya Kedang. Kwa mujibu wa nadharia ya mtazamo wa msikilizaji, tunaweza kufasili fomanti za chini za sauti zoloto na mamlaka. Kwa kawaida, sauti ya chini na nzito ndiyo hunasibishwa na nguvu na mamlaka tofauti na sauti nyororo au ya juu. Wahubiri kutumia sauti nzito kudhihirisha mamlaka ni jambo linaloweza

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

kueleweka katika muktadha huu kwa sababu ni lazima waonyeshe mamlaka waliyonayo kutoka kwa Mungu.

**Vigezo Vinginevyo vya Kubainisha Sauti Zoloto Kulingana na Wasailiwa**

Kutokana na mahojiano na hojaji zilizojazwa na wasailiwa mbalimbali, kuna sifa zingine za sauti zoloto ambazo ziliibuka.

***Mkwaruzo wa Koo***

Wahubiri wote waliohojiwa walidai kuwa sauti hiyo huwa na mkwaruzo wa koo, ni nzito na inag'ata ikilinganishwa na sauti ya maongezi ya kawaida. Pia, wahubiri watatu kati yao (waliozolota) walielezea kuwa sauti inapopita kooni, koo hukwaruzwa na hivyo sauti zoloto inatolewa. Wahojiwa watatu miongoni mwa sita walidai kuwa sauti zoloto husikika kana kwamba ni sauti ambayo imesukumwa kutoka mapafuni kama kikohozi. Mhubiri mmoja anayezolota alipohojiwa alidai kuwa sauti hii husukumwa kutoka mapafuni na ni vigumu kuitumia sauti hii iwapo mzungumzaji anapiga mayowe au anaimba. Hii yajibainisha katika mhimili wa nne wa nadharia ya mtazamo wa wasikilizaji, haiangazii tu kubadilisha mtindo wa utamkaji wa sauti bali pia uchaguzi wa jinsi ya kutamka sauti na upole wa mazungumzo. Hivyo, kutokana na mkwaruzo wa sauti za wahubiri wanaozolota, sauti hizo husikika kana kwamba hazina upole ikilinganishwa na sauti za wahubiri ambao hawazoloti kwani sauti zao hazina mkwaruzo wa koo hivyo husikika kana kwamba zina upole na utulivu.

***Toni ya Juu***

Pia, mtindo huu unapotumiwa, mzungumzaji hutamka sauti zake kwa sauti ya juu zaidi ikilinganishwa na utamkaji wa kawaida katika mazungumzo. Jambo hili linajikita katika mhimili wa nne wa nadharia ya Bell (1984, 1997) unaodai kuwa, mtazamo wa wasikilizaji hutumika katika viwango vyote vya lugha iwe ni lugha moja au wingi lugha kwani haiangazii tu kubadilisha mtindo wa utamkaji wa sauti bali pia uchaguzi wa jinsi ya kutamka sauti na upole wa mazungumzo. Hivyo, wahubiri wanaozolota huchagua wenyewe kuhubiri huku wakitoa sauti ya juu na nzito ikilinganishwa na mahubiri ya wahubiri ambao hawazoloti ambapo wao huongea kwa ukawaida na upole.

***Kipaji Kutoka kwa Mungu***

Wahubiri watatu kati ya sita waliohojiwa walibaini kwamba sauti hii ni kipaji kutoka kwa Mungu ambapo mhubiri hukipata anapozidisha mahubiri yake kwa waumini kwani jinsi anavyozidi kuhubiri ndivyo Roho mtakatifu ananena ndani yake. Kutokana na hali hii, wahubiri wanaamini kuwa waumini wao huvutiwa na huwashawishiwa na yale wanayoyahubiri. Hivyo basi, wanatumia sauti ambayo wanaamini waumini wa Kipentekosti wanatarajia na wanainasibisha na wahubiri wa madhehebu hayo. Hata hivyo, wahubiri watatu waliohojiwa haswa wale ambao hawazoloti hawakukubaliana na suala hili kwa sababu walidai kuwa wengine si kipaji kwani wao huiga wahubiri wenzao

***Mkao wa Mhubiri Anapozolota***

Kutokana na uchunzaji, ilibainika kwamba mhubiri alitumia sauti zoloto kwa wingi wakati ambapo alikuwa akihubiri huku ametulia bila ya kusongezasongeza sehemu za mwili wake au kutembeatembea jukwaani. Hii inakubaliana na tathimini ya utafiti wa Podesva na mwenzake (2015) walipodai kuwa sifa mojawapo ya utoaji wa sauti zoloto kwa wazungumzaji wote ni kuwa, hutolewa sana wakati ambapo sehemu za mwili hazisongasongi bali huwa pana utulivu mzungumzaji anapozungumza.

***Mwitikio wa Waumini***

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

Zaidi ya hayo, uchunzaji pia ulidhihirisha kuwa waumini katika ibada za wahubiri waliozolota walitoa mwitikio wa kupiga makofi, kutikisatikisa kichwa, kuwa makini zaidi na kuwa na mtazamo wa usikivu zaidi kuliko wakati ambao mhubiri hatumii mtindo huo. Hii ilijikita katika mhimili wa nane wa nadharia ya mtazamo wa wasikilizaji unaodai kuwa mtindo wa matumizi ya lugha katika uzungumzaji huwa chanzo cha mabadiliko katika mahusiano ya mazungumzo. Katika mhimili huu, vigezo tofauti vya lugha hutumiwa ili kubadili mitindo ya uwasilishaji wa ujumbe. Ilidhihirika kuwa jinsi mhubiri alivyotumia mtindo huu wa uzolotaji ndivyo lugha ilijisimamia, ikaongoza mawasiliano na pia ikaimarisha mahusiano ya mawasiliano kati ya mhubiri na waumini wake. Kwa kufanya hivyo, waumuni walielewa zaidi kuliko mahubiri ambayo mhubiri hakuhubiri akitumia uzolotaji.

## HITIMISHO

Makala haya yamejikita katika kuchanganua na kuwasilisha data kuhusu vigezo vinavyobainisha sauti zoloto zinazotumiwa na wahubiri wa Kipentekosti na umuhimu wake wanapowasilisha injili. Mihimili miwili ya nadharia ya Mtazamo wa Wasikilizaji ya Alan Bell (1984, 1997, 2014) ilitumika. Mihimili hii ilisaidia kubaini vigezo vinavyobainisha sauti zoloto inayotumiwa na wahubiri wa Kipentekosti wanapohubiri na utendakazi wake.

Vigezo vilivyotumika katika kuchanganua sifa za sauti zoloto miongoni mwa wahubiri wa Kipentekosti vilikuwa vitano: Kiwango cha Hz, urefu au ufupi wa mawimbi ya sauti, kuwepo au kutokuwepo kwa mpumuo, kiwango cha tambo, kipimo cha Fomanti ya kwanza na ya pili (F1) na (F2) na pia sifa kulinganaga na wasailiwa. Kutokana na sifa hizi, ilibainika kwamba sauti zoloto huwa na Hz ya juu inapotamkwa, muda wa kupumua huwa si wa kawaida na mawimbi ya sauti wakati uzolotaji unatokea huwa marefu ikilinganishwa na mawimbi ya kawaida mzungumzaji azungumzapo. Pia, mzungumzaji anapotumia sauti hii huwa ana mpumuo usio wa kawaida na hivyo kufanya mawimbi ya sauti kufululiza na kuwa na mizunguko mingi ikilinganishwa na mizunguko ya mawimbi ya uzungumzaji wa kawaida. Zaidi ya hayo, sauti zoloto huwa na F1 na F2 ya chini ikilinganishwa na F1na F2 ya sauti ambayo haijazolotwa. Hata hivyo, ilibainika kwamba sifa zingine za mhubiri ambazo huchangia sana katika utoaji wa sauti zoloto ni kama vile kutosongasonga kwa sehemu za mwili au kutotembeatembea jukwaani anapozungumza, nguvu sauti anazotumia wakati anapotamka sauti hizo, sauti zenyewe hunga'ta na huwa na mkwaruzo wa koo. Pia uelewa wa mada anayoishughulikia huchangia sana katika utoaji wa sauti kutoka kinywani mwake huku akitumia mitindo tofauti tofauti.

## MAREJELEO


Adam, M. (2017). Persuasion in Religious Discourse: Enhancing Credibility in Sermon Titles and Opening. *Discourse and Interaction*, 10, 2: 5-25.

Anderson, R. C., Klofstand, C. A., Mayew, W. J., & Venkatachalam, M. (2014). *Vocal Fry May Undermine The Success of Young Women in The Labor Market. PLOS ONE,* 9(5): e97506. doi:10.1371/journal.pone.0097506.

Bell, A. (1984). Language Style as Audience. *Design Language in Society*, 13, (2), 145-20

Bell, A. (1997). Style as Audience Design. In Nikolas Coupland and Adam Jaworski (Eds),

Sociolinguistics: *A Reader and Coursebook. London (pp.* 240–50). Macmillan.

Bell, A. (2014). Language when Contents Collapse: Audience Design in Social Networkings

*Discourse, Content & Media* 462-73.

Bellavance, S. R. (2021). Glottalization Variation in Young Speakers. Vermont University of Pennsylvania Working Papers in Linguistics,


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

27(1-3). https://repository.upenn.edu/pwpl/vol27/iss1/3

Belotel-Grenié, A., & Grenié, M. (2004). The Creaky Voice Phonation And The Organisation Of Chinese Discourse. International Symposium on Tonal Aspects of Languages: *With Emphasis on Tone Languages*, Beijing, China, March 28-31, 2004

Belotel-Grenié, A & Grenié, M. (1994). Phonation Type Analysis in Standard Chinese. *3rd International Conference on Spoken Language Processing* (ICSLP 94), Yokohama, Japana, Sept 18-22, 1994)

Brown, P. & Levinson. S.C. (1987). *Politness: Some Universals in Language Usage*. Cambridge:

Cambridge University Press.

Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. New York: Longman.

Esposito, L. G. (2015). I Am a Perpetual Underdog': Lady Gaga's Use of Creaky Voice in the Construction of a Sincere Pop Star Persona. Unpublished Masters Thesis. Swarthmore University

Gichuki, D. M. (2015). Conflict in Pentecostal Churches: The Case of Christian Church

International, Kiria-ini Town, Murang`a County, Kenya. Unpulished Masters Thesis.

Kenyatta University.

González, G., De Los Dngeles, M. & Sánchez, R.T. (2016). *English Pronunciation for Speakers of Spanish: From Theory to Practice*. Berlin, Boston: De Gruyter Mouton.

Hedelin, P. & Huber, D. (1990). Pitch Period Determination of Aperidic Speech Signals. *In International Conference of Acourstics, Speech and Signal Processing* (pp. 361-364).Held in Albuquerque, NM (April 3-5)

Hildebrand-Edgar, N. (2014). Creaky voice: An interactional resource for indexing authority.

Unpublished Masters Thesis. University of Crocker.

Holt, G. S. (1972). Stylin' Outta the Black Pulpit. In Thomas Kochman (ed.), Rappin' and

Stylin' out: *Communication in Urban Black America, (pp.* 189–204). Urbana: University

of Illinois Press.

Hornibrook, J., Ormond, T., & Maclagan, M. (2018) Creaky Voice or Extreme Vocal Fry in Young Women. *The New Zealand Medical Journal* 131 (1486), 36-40.

Keating, P, Garellek, M. na Kreiman, J. (2015). Acoustic Properties of Different Kinds of Creaky Voice.*18th International Congress of Phonetic Science*. Glasgow: Scotland.

Ladefoged, P. na Gordon, M. (2001). Phonation types: A cross-linguistic Overview. *Journal of Phonetics* 29, 383-406.

Ladefoged, P. na Johnson. K. (2011). *A Course in Phonetics.* Boston: Michael Rosenberg.

Lin, W. (2019). Three Modes of Rhetorical Persuation. *Sino-US Englsih Teaching* 16, 3: 106-112

Mahoney, R. (1993).*The Shepherds Staff.* Burbank: World Map Publishers.

McAlpine, A. (2016). An Examination of Vocal Fry as a Feminine Identity Marker. Academic Excellence Showcase Proceeding 47. https://digitalcommons.wou.edu/eas. Imepakuliwa Juni, 1, 2020.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1166

Møller, H & Pedersen, C.S (2004). Hearing at Low and Infrasonic Frequencies. *Noise and* Health, 6, 23, 35-57.

Mshvenieradze, T. (2013). Logos, Ethos and Pathos in Political Discourse. *Theory and Practice in Language Studies,* 3, 11: 1939-1945.

Naeem, M.H., Adleeb, N., Nadvi, N. A., Umar, M., Shabir, S.A. & Shabir, G (2014). Language of Religion. *International Journal of Innovation and scientific Research* 5, 1: 40-43.

Ndung'u, V. (2001). Uchanganuzi wa Usemi Katika Sajili ya Dini: Sifa Bainifu za Lugha ya

Mahubiri. Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Omowumi, A., Soku, D. (2015). Language Craft by Nigerian and Ghanaian Christian Preachers-

What Impact? *Double Blind Peer Reviewed International Research Journal* (vol. 15)

Podesva, Robert J. na Patrick C. (2015). Voice Quality and Identity. *Annual Review of Applied Linguistics* 35: 173-194.

Samely, U. (1991). *Kedang (Eastern Indonesia), some aspects of its grammar*. Hamburg: Helmut Buske Verlag.

Shaw, F. na Crocker, V. (2015). Creaky Voice as a stylistic feature of young American female Speech: An intraspeaker variation study of Scarlet Johanson. *Lyfespans & Styles: Undergraduate Working Papers on Intraspeaker Variation*, 1: 19-27.

Similly, L. (2012). Make it Happen Preacha: African American Rhetorical Licence, African American Vernacular Englsih (AAVE), and a Modern Rendering of Epideictic Rhetoric. Unpublished PhD Dissertation. University of Texas.

Sorokowski, P., Puts, D., Johnson, J., Zoleklewicz, A., Oleszklewicz, A., Sorokowska, A., Kowal, M., Borokowska, A & Plsanski, K. (2019). Voice of Authority: Professional Lower their Vocal Frequencies when Giving Expert Advice. *Journal of Non-Verbal Behavior* 43: 257-269.

Smithermann, G. African American Englsih: From the hood to the Amen Corner. Keynot Speech Presented for the Center for Interdisciplinary Studies of Writing 1995 Conference Linguistics Diversity and academic Writing. University of Minnesota.

Taylor, G. C. (1977). *How shall They Preach.* Elgin.IL*:* Progressive Baptist Publishing House.

The Bible societies (2008). *Holy Bible.* Revised Standard: China. Bible Society Resources Limited.

Tumbull, R. (1967). *Baker's Dictionary of Practical Theology.* Grand Rapids: Baker Book House.

Waweru, T. W. (2014). Matumizi ya Lugha Katika Kanisa Katoliki: Uchanganuzi wa

Ubadilishaji Msimbo Katika Mahubiri. Tasnifu ya Uzamili Haijachapishwa. Chuo Kikuu

cha Nairobi.

Wolk, L., Abdelli-Beruh, N na Slavin, D. (2012). Habitual use of Vocal Fry in Young Adult Female Speakers. *Journal of Voice,* 26(3), 111-116.

Yuasa, I. P. 2010. Creaky Voice: A New Feminine Voice Quality for Young Urban-oriented Upwardly Mobile American Women? *American Speech* 85:315-337.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.